JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI OSHARA
S. L. P 31
SIHA
25.4.2024

Namba za simu

- Mkuu wa shule 0755 883 008
- M/mkuu wa shule 0766 642 700
- Matroni 0714 229 664
- Mwalimu msajili 0626 454 006

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI OSHARA ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA MKOANI KILIMANJARO MWAKA 2024/2025.**

Nafurahi kukutaarifu kuwa, mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule sekondari Oshara, iliyopo wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro jirani na Hospitali ya Taifa ya Kibong'oto.

## 1. MAHALI SHULE ILIPO.

Ukitokea Moshi mjini panda gari linaelekea Sanya juu shuka kituo cha **Lawate** kwa nauli va Tsh 2500, kisha waweza chagua usafiri binafsi kati bajaji Tsh 2500 au pikipiki Tsh 2000 kuelekea shule ya sekondari Oshara. Ukitokea Arusha shuka Bomang'ombe kisha panda gari la kuelekea Sanya - Juu na shuka kituo cha LAWATE, kisha waweza chagua usafiri binafsi kati ya bajaji Tsh 2500 au pikipiki Tsh 2000 kuelekea shule ya sekondari Oshara.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **1 Julai 2024** hivyo mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **1 Julai 2024**. (Kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi kamili) Mwisho wa kuripoti ni tarehe **8 Julai 2024**.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 . SARE YA SHULE

i. **SKETI MBILI** — Rangi ya **KIJANI ST LOUS/PIPI KALI NAMBA 1039** aina ya mshono ni rinda box ndefu chini ya magoti (urefu usiopungua 6cm kuanzia katika magoti kuelekea katika kifundo cha mguu au zaidi).
ii. **Sweta** walau moja ya rangi ya KIJANI iliyofanana na sketi ya shule, tai ya kijani yenye mistari meupe.
iii. **SHATI MBILI** — Rangi nyeupe mikono mifupi
iv. Sare ya michezo kwa Shule hii ni - sketi 2 ya rangi ya Orange inayofika katika magoti (solo)
   - Tshirt ya rangi ya blue yenye nembo ya bendera ya taifa (jezi) pamoja na bukta yake na viatu vya michezo (raba)

v. Viatu vya Shule viwe vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
vi. Soksi jozi mbili au zaidi ziwe nyeupe.
vii. Nguo za kushindia mbili drafti ndogo ya rangi ya purple na nyeupe mshono wa solo ndefu yenye kitambaa cha ndani (lining).

viii. Track suit moja ya rangi nyeusi na sweta za ziada mbili kujikinga na baridi rangi ya dark blue au nyeusi pia anaruhusiwa kuja na pullneck rangi nyeusi au nyeupe.
ix. Madaftari makubwa 3 QUIRÉ saba.
x. Mabuti (Rain boot)
xi. Ream mbili (2) ya Karatasi nyeupe aina ya A4 iliyoandikwa **PAPERLINE MULTIPPURPOSE PREMIUM PAPER**

NB:

- **HAIRUHUSIWI KUSUKA NYWELE**
- **MWANAFUNZI YEYOTE ATAKAYEKIUKA MAELEKEZO YA MISHONO YA SARE ZA SHULE MZAZI ATA WAJIBIKA KUSHONA SARE NYINGINE**

**2.2 MICHANGO VA SHULE**

| | | |
|---|---|---|
| i. | MICHANGO YA UENDESHAJI WA SHULE 65,000/= | |
| ii. | TAHADHALI | 5,000/ |
| iii. | NEMBO | 5,000/= |
| iv. | KITAMBULISHO | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

NB: KILA MZAZI AHAKIKISHE MWANAE ANABIMA YA AFYA (NHIF) NA NI LAZIMA.

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
v.Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nyweie fupi wakati wote wawapo shuleni.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moia, kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za sta^r,ehe na nyumba za kulala wageni;
XV. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya Shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanyajaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4.VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

(a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.

(b) •Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa yajinai.

(c) ) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

(d) Kopi ya cheti cha kuzaliwa na Kopi ya result slip

4. TAFADHALI SOMA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYAFUATA.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU

Saini ya Mkuu wa shule....... ………

Jina la Mkuu wa Shule YUKUNDA R. LYIMO
MKUU WA SHULE

Mhuri wa mkuu wa shule.. …………………..

C. **MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI**;

i. Sanduku la bati lenye kufuli kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake.

ii. Mashuka pair mbili rangi ya pinki, blanketi moja, foronya mbili, chandarua moja nyeupe au bluu.

iii. Godoro upana futi mbili na nusu kwa inch 3 (inapendekezwa TANFORM au COMFY)

iv. Ndoo mbili ndogo zenye mifuhiko,

v. Sabuni ya kuoshea choo aina ya DEX NZITO YA MAJI LITA TANO au DISINFECTANT,

vi. Brush ngumu 2 zenye mpini mrefu,

vii. Moper 2 zenye mipini mrefu

viii. Slesha (fyekeo) moja

ix. Fagio za chelewa 2

x. Vyombo vya chakula (kontena lenye mfuniko) kijiko na kikombe.

VJTABU; Mzazi/Mlezi unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu vitakavyomsaidia katika rejea na baadhi ya v;tabu hivyo ni kama;

AINA YA KITABU

| SOMO | |
|---|---|
| GEOGRAPHY | Practical Geograpy by Zist Kamili [D. T. Msabila<br>Approach to physical Geo questions by Ahmed Lumbwana,<br>Research methodology by Cothary<br>Geo ra h a er two b Msabila |
| GENERAL STUDIES | Understand General studies for advance level by JOHANES BIGIRWAMUNGU & STEPHEN |
| KISWAHILI | Nadharia ya Lugha kidato cha 5&6 kimeandikwa na Masebo ambari |
| | vance eve 1Story —<br>Essential in advanced History by SALEH MASSIN<br>Mastering A-level History paper 1&2 |
| KIINGEREZA | - eve ng approaci y I<br>Comprehensive course in A-level literature stylistic and communication skills.<br>Public speaking for collage and carrier by George .H<br>The wonderful surgeon C.M!oka.<br>Theory of literature by Nyambari -I |

N.B Pia anaweza kuja na vitabu vingine kwa kadri atakavyoona

FOMU NAMBA 0I NA 02 ziwasilishe kwa msajili mara ufikapo shuleni

## 5. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Efimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elirnu, Sayansi Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais — TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji; wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo. ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

5.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine najamii kwa ujumla ni jam la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za Shule utokazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya Shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi ivako katika Shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na maz:ngira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapoQkiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za Shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kaii na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawa shuleni.

MUHIMU:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna- mtumishi anayeruhusi\vh• kutuy
simu ya mwanafunzi;

- Mwnnafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni a!ilopangiwa na kitanda alichopangiwn. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiv Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maaJum toka kwa Mkuu wa Sh!lle. (Msiba au Ugonjwa).

wa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa akitumiwa ujumbe mfnpi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walirnll na kuwa toto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mabututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI PATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USI i'UME CHOCHOTE, NI VEM
KAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAAIUFA HUSIKA KWA NAMBA [FUATAZO: -

| | |
|---|---|
| > Mkuu wa shule | 0755 883 008 |
| > Makamu Mkuu wa Shule | 0766 642700 |
| > Mwandamizi Taaluma | 0626 454 006 |
| > Mwandamizi Malezi | 0714 229 664 |

F01

FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUMUSU HISTORIA YA MWANAFUNLI/MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA
MGOMO, FU.JO NA MAKOSA YA JINAI

NA RIDHIO LA MZAZI/MLEZI

Mimi (MAJINA YA MWANAFUNZI)…………………………………………………….

Mzaliwa wa mkoa………………….wilaya ya……………kata ya…………tarehe ya kuzaliwa……..

Namba ya wazazi au walezi……………………………………………….

Makazi ya wazazi au walezi (wakati wa likizo) mkoa…………………………..wilaya………………

DINI au MADHEHEBU YA WANAFUNZI………………………………………………………….

i. Naahidi kuwa mwaminifu na mtiifu kwa sharia na kanuni za shule na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
ii. Nakubali kuwajibishwa kama nitaenda kinyume na kanuni na sharia za shule kwa muda wote nitakapokuwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Oshara nje au ndani ya shule
iii. Nitakuwa mwenye nidhamu ya hari ya juu ya kusoma kwa bidii ili kufanikisha malengo ya ufaulu
iv. Nitakuwa mzalendo , nitalinda hadhi, heshima ya shule popote kwa uaminifu.

SANI YA MWANAFUNZI.......

v. Mimi mzazi/ mlezi Nimesoma na kuelewa kanuni na sheria za shule na naahidi kuwa nakubali kushirikiana na Uongozi na Jumuiya nzima ya Oshara katika malezi ya mwanafunzi tajwa hapo juu ili kufanikisha taaluma yake kwa manufaa yake na Jamhuri ya Muungano ya Tanzania

Naahidi nitatoa ada na michango ya shule kadiri ilivyoelekezwa.

SAİM YA MZAZI/MLEZI…………………………………………………………

MAJINA YA MZAZI /MLEZI ……………………………………………………………

F02

PRESIDENT OFFICE
REGIOAL ADMINITRATION AND LOCAL GOVER NMENT
SIHA DISRICT COUNCIL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINA
TION

PART ONE

NAME OF THE STUDENT..............................................................................

Please examine the above named person as to be admitted to advanced secondary school education at Oshara High School

Name of the head of school YUKUNDA R. LYIMO HEADMASETER

Blood account (red & white) …………………………stool examination………………...

Urine.........................................................................analysis……………………………………………..

T.B. test ………………………………Eye test …………………Ears test ……………………………

Abdomen test ……………………………………chest test………………………………………

Spleen test ……………………… Pregnancy test..... ........................................................................

Addition information……………………………………………………………………………………

……………………………………………………… ……………………………………………… ……

Infection, chronic or family disease
……………………………………………………………………………………………………………

Please, I certify that the above named student is fit to be at OSHARA SECONDARY SCHOOL

SIGNATURE............... ...……………………………………………………………………………………

Designation... . . . . . . . . . . . . . . . . . . . ……………. . Station……………………………………………………

Date.... . . . . . . . . ..………………………

Kabidhi fomu hii ikiwa imejazwa kwa msajili mara tu unapofika shuleni.